
**Elong'o Publishers Online Bookstore eBook**

**This eBook has an embedded link that helps us track it, it is not for sharing or posting online.**



# CHOZI LA DAMU

# Washington Bin Juma

# CHOZI LA DAMU

**Haki zote zimehifadhiwa**

Nakala hii hairuhusiwi itolewe kwa njia yoyote ile kama vile kuichapisha tena au kuhifadhi kwa njia ya kieletroniki wala kuitumia bila ruhusa kutoka kwa mhariri ama mwandishi.

Toleo la kwanza: Machi 2021

Kimechapishwa na Elong'o Publishers

**ISBN: 9798720827632**

**Washington Bin Juma**

**Simutamba: +254717797486.**

Baruapepe: jumaezekiel509@gmail.com

**Mhariri**: Kaka Fred.

**Simutamba** : +254716349065

# UTANGULIZI.

Chozi la Damu ni kazi iliyosawiri matukio ya hali halisi yanayotokea katika jamii zetu. Riwaya hii itakupa taswira tosha kuhusu namna mazingira yanavyochangia kuendelea au kufeli kwako katika maisha. Malengo yamesawiriwa vilivyo ili kumpa msomi yeyote mbinu chanya ya kukabili maisha. Asilimia kubwa ya waja hukata tamaa pasi na kujua kuwa baada ya giza ni nuru. Nilikitunga kwa ajili ya kukuza lugha ya Kiswahili inayotumika sana katika nchi ya Kenya, Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi, Afrika ya Kati, Afrika Kusini na kwingineko duniani.

Utawapata wahusika wawili wanaojitegemea kuishi haswa baada ya kuhama kwatika makazi yao ya majadi kubeli na kuishia kuishi katika kibanda kimoja. Je, kipi kikichosabisha wao kujikuta katika hali hiyo? Pata ufahamu kwenye kisa hiki.

Riwaya hii itakupa nuru kuhusu majanga yajayo pasipokuwazia wala kutarajia. Isitoshe, msomaji atapata ufahamu kuhusu sababu zinazowafanya watoto wadogo kujikuta katika matatizo fulani haswa baada ya kukaidi amri ya wazazi wao.

Wa'Salaam!

**Washington Bin Juma**

Akiwa **amegona** na kugunjama kichalichali kwenye kitanda chake cha akina pangu pakavunitilie mchuzi, Bi Katembo alijikuta kwenye mujarabu akikaribishwa kwa upwamu na uchangamfu kwenye shamba la ndoto akikumbuka na kudhukuru bayana na kinagaubaga kilichojiri usiku huo wa Alhamisi. Mumewe Bw. Katembo ambaye amekuwa akizumbua riziki katika nchi jirani ya Uganda, akirejea mastakimuni mida ya saa tatu hivi za usiku mchanga.

Kinyume na kawaida yake, leo hii alifika pasipo kumfahamisha wala kumjuvya mkewe. Mjo wake ulipokelewa na vijibwa vyake viwili vilivyomkaribisha ingawa mwanzo viliyatishia maisha yake kwa kudiriki kumng'ata. Viligundua kuwa hakuwa **ajinabi** ila mwenyeji. Bw. Katembo alionekana akinyong'onyea kwa mavune na machovu si kidogo alipopokelewa na kukongowewa na mkewe kwenye hicho kibanda cha msonge.

Bi Katembo aliendelea kuota. Kilichoonekana kwenye makazi haya ni taswira na ithibati tosha ya jamaa inayogandamizwa na kugugunwa na urumo, uchochole, udhikifu na ufakiri wa sina sinani; pembeni mwa kibanda hiki karibu na kijidirisha, kuna kijimeza kidogo hivi kilichoonekana kuundwa kwa makuti yaliyounganishwa na kushonwa kwa kutumia katani. Aidha, kilizungukwa na mawe matatu hivi yaliyochimbwa mchangani. Ukiniuliza sitachelea kukuambia kuwa ndivyo viti vyao. Hatimaye aligutuka usingizini. Bi Katembo aliangazaangaza huku na huko ila hakuelewa maana ya ndoto hiyo. Kulikuwa na kijimeza kidogo pembeni.

Juu ya kijimeza hicho kulikuwa na **kibahaluli**. Hicho kifaa kilionekana kikiangaza kwa mwangaza na nuru hakiri na dhalili hivi.

Aina ya taa sampuli hii katika familia nyingine zilipitwa na wakati lakini kwa Bi. Katembo, ni sawa na ganda la muwa la jana ambalo chungu huona kivuno.

Dirisha nalo si dirisha jinsi unavyotaamuli. Kinachoonekana ni fukuo au kijishimo kidogo kwenye ukuta wa mashariki ya kijumba hiki. Wakati wa kutwa huwa wazi lakini ifikapo usiku, hujazwa matambara na marapurapu. Huenda kwa nuio na gharadhi ya kuwakingamanisha wadudu hatari wakiwemo mbu, sisemi vijoka na vile vijipanya.

Kutani palionekana viumbe hai waliotembea na kunyendea bila hofu wala **kokoneko** yoyote. Si kombamwiko si kereng'ende si buibui si mjusikafiri si vijipanya. Ukiwaona utadhani ama wanamkaribisha Bw. Katembo nyumbani au yamkini wanajitafutia riziki kutokana na masazo au makombo ya jioni hiyo. Jambo ambalo ni ibra madhali iwapo humu msingeonekana chochote cha kuonja seuze kile cha kumeza?

Viambaza vyenyewe navyo vilichangia kuendeleza maudhui ya utwea wa hali ya juu. Vimekandikwa na kubandikwa kwa mchanganyiko wa samadi na tope. Ungeshindwa kubaini iwapo hii ilikuwa samadi ya ng'ombe, punda, nguruwe au sijui niseme nini? Harufu, riha na kinyaa kinachoyahinikiza mandhari haya ni ya kukirihisha na kukefyakefya maradufu ya harufu ya ule mzoga wa mbwa au harufu inayosababishwa na mjambo au mnyambo wa punda. Ashakum si matusi.

Nayo sakafu aidha iliyokandikwa kwa samadi hii hii imesheheni mashimo mengi ajabu. Sielewi iwapo haya ndiyo makao ya hivi vidudu au vipi? Mlango wa kichumba chake ulikuwa sawa na karatasi ya sandarusi au plastiki zilizogugunwa na mchwa. Kijilango chenyewe kilitengenezwa kwa vijibati vilivyounganishwaunganishwa na

kubandikwa pamoja kwa nyaya za stima. Sijasema walikuwa na stima! Ajabu na ibra ya Firauni ni kuwa kijilango hiki kinafungwa kwa msumari mmoja tu!

Chumba cha malazi na hiki cha makaribisho, vilitenganishwa na pazia moja kuukuu, kongwe na **kadimu**. Ni muhali kubaini rangi yake halisi kwani ilisheheni mapakumapaku na mapachumapachu ya sijui uchafu ama rangi yake halisi. Kile kichumba kilikuwa ndio mazingira mapya ya Bi. Katembo. Alikaa mle pekee kwani mumewe alikuwa kikazi kule Uganda. Kuna maandishi yaliyokuwa kwenye ukuta wa kichumba kile. Kwa tabaradi, Bi. Katembo aliyasoma tena kwa mara nyingine maandishi yale yaliyoibua mjadala na mdahalo mwingine tafakurini mwake; "*UKITAKA KUISHI MAISHA YA AMANI, UTUVU NA USALAMA MUULIZE MASKINI*" ingawa hakuelewa dhamira na azimio la aliyoichora nadhari hii ya herufi. Mawazo yalijaza uketo wa akili zake. Hatima ya mawazo hayo ilitia nanga baada ya kuibiwa tena na lepe la usingizi punde tu alipoizima koroboi yake.

Asubuhi ilipofika, alitembelewa na rafikiye waliyesoma naye. Yule sahibu yake alishangaa kumkuta Bi Katembo katika mazingira yale.

"Shoga yangu, mbona ulibadili mazingira ya awali na ukahamia huku kwa mazingira mabovu hivi?" Rafikiye alishangaa. Bi Katembo alimsimulia kisa kilichomleta katika mazingira hayo kimasomaso na kinagaubaga.

"Rafiki yangu unayoyaona ni jibu la yale yaliyotokea. Waneni walisema, chungu kipikapo mifupa huvunjwa na mifupa. Kama unavyojua tulikuwa tukiishi Kapweta katika jumba letu la kifahari. Siku moja usiku wa manane, kama ujuavyo ndio uliokuwa muda mwafaka wa

wawanga kusafisha na kukosoa misheni yao kwenye kilinge chao. Usiku ambapo anga ilikuwa imetabaradi na **kustakiri** kwa ukimya wa ajabu, hata vyura walioishi kuwatumbuiza, kuwaliwaza, kuwaburudisha na kuwastarehesha wakazi kwa sauti zao za mighuno, hazikusikika kokote abadan kataan. Kimya kingi kina siri! Kwa kipindi cha siku tatu hivi, mvua ya kidindia ilikuwa imekunya na kunyea kwa mtawalia na mfuatano bila kutanzuka wala kupusa.

Maji yalituama kwenye mashamba, nyanjani, vidimbwini na pembeni mwa vijia ungedhani ni kifungulima jangwani. Migunda na makonde yaliyoandaliwa zaidi ya miezi mitano sasa, yalijaa maji, kupuka na **kusarasara**. Aidha, kuna yale yaliyopata makao kwenye migodi, mahandaki na mashimo. Kuna duru za kuaminika kuwa yapata miaka zaidi ya miongo miwili iliyopita, palizuka uhasama na utesi kwenye eneo hili la Kapweta baina ya jamii mbili tanzu kutokana na sababu za unyakuzi wa mashamba na wizi wa mifugo. **Adharusi** hiyo ilisababisha maafa mengi. Jambo lililoifanya serikali kuingilia kati.

Hii ndio iliyokuwa sababu ya haya mahandaki kwani yalichimbwa na walinda usalama waliotumwa na serikali kushika doria na kuimarisha amani na usalama katika eneo hili la Kapweta. Maji hayo yalijenga makao mufti kwa wadudu waliosababisha hatari kwenye maisha ya wakazi wa Kapweta. Wadudu waliozua hawafu ni mathalani; Mbu, Mbung’o na Nge. Wadudu hao walichangia asilimia kubwa ya **mauko** kwa wakazi wa Kapweta.

Ni jambo la kuhuzunisha na kustaajabisha madhali kila baada ya miezi sita, serikali ilikuwa ikiwasambazia vyandarua vya kuzuia Mbu. Ni kinaya kikubwa unapopita katika baadhi ya vijishamba,

kinachoonekana ni stihizai na tashtiti ya kufedhehesha kuona vyandarua vivyo hivyo vimetumika kama **mafaja** ya kuyazungushia mashamba. Kipindi hicho cha mvua ya kidindia, kilisalia funzo la mjinga kwa wanakapweta kwani serikali ilidinda kuwauni vyandarua kutokana na ubwete wao wa kuvitumia visivyo. Kumbe mwiba wa kujidunga huambiwi pole. Istoshe, walichelea kumaizi kuwa siku utakapokwenda uchi ndiyo siku utakapokutana na mkweo. Viongozi wengine walijaribu kumrai rais wao ila ilikuwa sawa na kumpaka nguruwe hina wakati unajua vizuri kuna kidimbwi cha tope. Ili kuepuka janga hili ilitubidi tuhamie huku katika chumba hiki cha kukodi. ". Bi Katembo alikamilisha kisa chake kilimfanya kutiririkwa na machozi ya majonzi. "Kwani vyombo vya samani na hivyo vya elektroniki mliviacha kule?" Rafikiye alimuuliza. "La hasha kipindi kile kikiendelea, ilitubidi tuviuze ili tufidie mkopo maana mume wangu alikuwa amechukua kwa nuio ya kuutumia kwenye upanzi. Kwa kuwa hatukuwa na namna ya kujisetiri, ilikuwa Faradhi tuuze vyombo ila nyumba ikasalia. Hakuna mnunuzi aliyekubali kuinunua kitokana na sifa za mazingira mabaya ya kijiji hicho" Bi. Katembo alisawazisha.

Baada ya kula staftahi, Bi. Katembo aliendelea kumjuza mwandani wake namna maisha yalivyokuwa Kapweta. Alimfahamisha kuwa wenyeji wa Kapweta hawakuhitaji ulinzi wowote; uwe wa polisi au wa mabawabu. Wenyewe walijitwika dhima ya kuwajibikia usalama wa kila mkazi. Hapa kwao msamiati kama: bawabu, kufuli, mlango, nyua za stima, malango ya vyuma na majibwa ya ulinzi ni msamiati usiopatikana katika kamusi yao. Ni muhali mithili ya maziwa ya kuku kuvisikia visa na viroja kama vile wizi wa kuku, wizi wa mazao shambani, wizi wa benki, ubomoaji wa maduka; Ajabu ya maajabu ni kuwa hili ndilo eneo pekee ambalo benki, maduka madogomadogo na

yale makuu huachwa wazi bila kufungwa iwe usiku uwe mchana! Visa hivi katika eneo hili la Kapweta vilikwishazikwa katika kaburi la **mghafala**.

Muda wa sahibuye ulitamatika. Alipoondoka, alimuacha mwandani wake akiungaunga maisha katika Kijiji chake kigeni. Maisha hayo yalimfanya atokomee katika njia mbadala kwani hata mumewe alishindwa kuyakimu maisha yake kutokana na kufidia ule mkopo.

Siku moja alikuwa ametulia kwenye kivuli cha mti wa mwarubaini. Akaanza kukumbuka jinsi mumewe alivyomfumania na hawara wake siku moja. Alichokifanya Bw. Katembo siku hiyo ni yakini yakinifu kuwa ni vigumu na muhali sana kumpata mwanamume jinsi hii hasa katika Bara hili la Afrika. Kitendo hicho kilisalia jeraha lenye machungu yasiyokuwa na utando moyoni mwa Bi Katembo. Bi Katembo alitarajia adhabu ya mbwa aliyeingia msikitini lakini kikawa kinyume kabisa na tazamio lake! Kwani Bw. Katembo alimtazama mkewe kwa uso mkunjufu, kicheko na mteremo kinyume na alivyojulikana. Sijui iwapo hiki kilikuwa kejeli au vipi? Alimgeukia kimada wa mkewe akamsabahi na kisha kumpa kibali cha kuondoka jinsi alivyoingia. Kimada yule ndiye aliyempa mahitaji yake ya ngwenje. Mkewe alitarajia kipindi cha makonde na mateke lakini ng'o! 'Maajabu haya' , alijisemea kimyakimya. Bi Katembo aliendelea kubukua matopa ya kumbukumbu yake. Aliyakunjua yote yaliyojiri kutoka **ukoko hadi ulando** baada ya tukio hilo lililojaa tahayuri, soni na **junaa**. Aliuhisi mtima wake ukitona matone ya damu. Damu ya machozi. Milizamu njia nne nne ilimtiririka na kumnyiririka mashavuni. Haya si machozi ya mamba! "Nani angemwondolea lawama hii?" Dunia! Dunia! Dunia! Aliamshwa na mkirizo wa simu yake. Kumbe ilikuwa simu kutoka kwa mumewe

aliyekuwa akimjulia hali. Baada ya mazungumzo ya muda aliendelea kupunga unyunyu kwenye kivuli cha mti huo.

Mabadiliko mengi yalionekana wazi kwa Bw. Katembo. Hakuna siku aliyowahi wala kuthubutu kumkumbusha mkewe kuhusu tendo hilo. Badala yake, aliuzidisha upendo kwa mkewe. Akayakidhi mahitaji yote bila kuchelea wala kusaza lolote. Mara si moja haswa siku ya Jumamosi, akamtembeza sehemu mbalimbali za burudani na maonyesho. Si Lokichogio, si Juba, si Torit si Kakuma. Almuradi wakawa na nafasi murua ya kuzibwaga nyoyo zao.

Hata hivyo, licha ya mabadiliko haya yote, Bi. Katembo hakuridhika wala kuridhia. Alijawa na jakamoyo si haba. Hali hii ikamfyonza na kumguguna akabaki **kifyefye**. Moyoni aliendelea kushuku kuwa yamkini mumewe ana njama fiche aidha ya kujiangamiza au kumwangamiza. Mambo ni mawili!

Usingizi ulimchukua alipokuwa kivulini. Alipokuwa amezaka kwenye lepe hilo, aligutushwa kwa maumivu ya kucha za vijibwa vyake vikivyokuwa vikimrukiarukia. Mwili wote ulilowa jasho rovurovu. Moyo ulimrindima; mwili si wake tena. Aliyafikicha macho na kuhakikisha kuwa yupo kwake, macho yake yalikutana ana kwa ana na yale ya mumewe. Kumbe ndoto hii yote ilipokuwa ikijikunjua na kuchukua mikondo ya kutisha, Bw. Katembo alikuwa pia kwenye safari yake ya kumkagua, kumchunguzachunguza na kumsomasoma mkewe kama mtu asomavyo kitabu chenye michoro ya viumbe hai na wafu. Mara akamkagua miguu, mara uso, mara pua, mara mdomo, mara mikono, mara nywele, mara meno, mara masikio, mara shingo, mara kucha. Sikwambii sehemu ya mbele ya kidari!

“Mume wangu, mbona umenitundulia kiasi hiki cha kunitia hofu. Mbona hukuniambia kuwa waja?” Bi Katembo akamsaili.

“Sina nia yoyote mbaya mke wangu. Nilipokupigia simu nilikuwa supamaketi. Usihofu mtazamo wangu ila nimekuwa nikiyafurahia maumbile yako yenye urembo wa mvuto na mnato tu!” Bw. Katembo akamjibu.

“Mimi sina undani wowote wa moyo mwenzangu” akasisitiza. Haiya karibu nyumbani. Habari za utokako? Bi Katembo alimkaribisha. "Asante sana mke wangu. Nitokako kwema kazi nzuri maana miezi miwili ijayo nitakuwa naumalizia mkopo wangu", Bw Katembo alimjuza. Waliendelea na utani wao.

"Huu upendo wa kizazi cha leo ni wa ulimwengu na malimwengu uliojaa mizungu, mauzauza na mazingaombwe. Ajabu ya maajabu ni kuwasikia wengi ambao hawajafunga akidi wakilonga na kusogowa kuwa asilimia kubwa ya wanandoa huwa na maisha ya asali na maziwa. Mara tu wavukapo kizingiti cha ujana na kuoa na kuoleka, mtazamo na mwangalio huu huchukua mkondo mwingine. Wao hao ndio utawasikia wakighilibika na kugereshwa kuwa maisha ya ukapera na uanawali ni ya starehe, nyemi na yenye uhuru! Ndicho kinaya cha maisha" Bw. Katembo alimtarifu mkewe.

"Mbona sikuelewi? Hizi ni baadhi ya falsafa potovu zilizopitwa na wakati na kuzishikilia kikiki ni sawa na kujigeuza **chanduchandu** anayejipalia makaa. Aghalabu mawazo haya ndiyo yanayochangia pakubwa mmomonyoko wa uaminifu baina ya wanandoa. Mahusiano sampuli hii sharti yapigwe vita kwa ujino na ukucha lama yaangamizwe" Bi. Katembo alijitakasa.

Mazungumzo yao yaliteka paa na kuhanikiza kote. Mwana akibebwa hutazama kisogo cha nina yake. Ni wazi na dhahiri kama jua la utosini kuwa watoto aghalabu huzifuata nyendo, silika, hulka na tabia za wazazi au walezi wao, ulumbi huu unazalika, kumea na kuota mizizi kutokana na maisha ya Bi Katembo. Hii ni miaka minne baada ya kisa kilichompata. Kumbe mambo kangaja huenda yakaja. Waliekea chumbani huku mikononi wamebeba boksi zilizojaa bajeti.

Ni majira ya alasiri kama saa kumi hivi, Bw Katembo na mkewe walikuwa wametulia kwenye kiti cha gogo nyuma ya kibanda chao. Punde kabla ya kuzamia katika mazungumzo yao, rafiki yake Bi. Katembo aliwasili. Bi  Mwaipaji alikuwa sahibu wa muda mrefu sana na Bi Katembo. Uso wake ulisawiri mapya ambayo shoga yake hakujua. Aliwasimulia masaibu yaliyomkumba

Ng'andu mwanawe, pamoja na Sijali, walienda kwenye mto Kapchembo kuogelea. Hiyo ilikuwa ada yao. Wawili hao walikuwa marafiki wa toka nitoke au niseme **usuhuba** ule wa dhati ya moyo. Uhusiano huu ulizalika kutokana na usena kati ya wazazi wao pamoja na kuwa wote walisomea shule moja ya msingi humo kijijini mwao. Sijali alikuwa mwanambee wa Bi Katembo naye Ng'andu alikuwa mziwanda wa  Bi. Mwaipaja. Bi. Mwaipaja na Bi. Katembo walikuwa **mbasi**  wa kipindi kirefu. Pengine ningesema ni wale wa nifae kwa jua nami nikufae kwa mvua. Aidha, wao ni majirani wa pua na mdomo. Kuntu, wanaifahamu falsafa isemayo, "Ujirani mwema hutengeneza njia. Ama wengine wangesema, ujirani ni fedha katika kasha".

Kabla ya kuanza kuogelea na kupiga kachombe, Abdallah na Bakari wanafika na kujiunga nao. Kwa zaidi ya saa moja wamekuwa

**wakiovodha** kwa upwamu na hanjamu bila tahadhari yoyote. Hawakujali madhara na mauja ya hayawani hatari kama vile majoka, mamba na viboko ambao haya ndiyo makazi yao kwa miaka mingi.

Mara kwa mara wamekanywa na wazee wao dhidi ya kushinda kwenye eneo hili hatari hadi mida hiyo ya machweo, lakini wote waligeuka sikio la kufa ambalo tangu lini likasikia dawa wala kafara? Si mara moja si mara mbili wameadhibiwa kwa **mirapuo** isiyo na hesabu lakini ajabu ni kuwa wamekuwa jabali kustahimili vishindo vya ufito. Waama, mwana mkaidi hafaidi mpaka siku ya Idi.” Bi. Mwaipaja aliendelea kuwasimulia.

"Saa moja baadaye walikinai kuogelea kisha wakanuia kurejea nyumbani. Akrabu ya saa iliyoonyesha saa moja kasoro dakika kumi. Walipoitazama na kutupa macho kule walikokuwa akina Abdallah na Bakari, hawakuwaona wala kupata fununu zozote. Walipigwa na **mduwalifu** walipoyakosa mavazi yao yote walipokuwa wameyaficha! Walitafuta kwa zaidi ya nusu saa ila wakaambulia pang’anda. Hii ikawa sawa na juhudi za mfa maji. Hapo ndipo walipobainikiwa kuwa nguvu za mayonda hufilia nyangwani.

Yakimwagika yamemwagika na katu hayazoleki. Kilio cha vyanda vili kinywani kisingewafaidi chochote wala lolote. Sijali akashauri waanze mwendo japo katika hali hiyo hiyo ya rabana na tupu. Maskini! Ole wao watoto wa Adamu. Wanaonekana wakinyatanyata na kunyendeanyendea kwenye uchochoro unaokata katikati ya mgunda wa migomba ya ndizi. Shamba hili limeshiba mmea huu hadi linatishia kutapika mingine" Bi Mwaipaja alisimulia. "Maskini wanangu! Ikawaje shoga yangu?" Bi Katembo alishtuka akadakia.

"Giza la kaniki na la kuogofya lilipovaa anga, vijana hawa walikuwa bado hawajafika nusu ya shamba hili. Sijali alimshika na kumgandia Ng'andu mkono wa shimali. Mwendo ni ule wa furukombe huku roho **zikiwapapa** na kuwarindima kama ngoma ya msondo. Waliwakumbuka marafiki zao – Bakari na Abdallah. Mbona wakaondoka kimyakimya bila kuwataarifu? Ama wao ndio waliowatendea **ubedui** na uhabithi huu? Wakadiriki kuwalaumu lakini vinywa vikawazuia baada ya kujiasa.

Dakika hamsini baadaye ziliwafikisha kwenye gurufu – Njia kuu. Baada ya mwendo wa dakika kadhaa hivi, walibeta kushoto. Ghafla malaika yakawasimama tisti, damu ikawasisimka na kuwachachatika. Miguu ikawalegea legelege kama utumbo wa samaki. Ukete na utengemano uliokithiri usingewaruhusu kupuma, kupumua wala kutweta. Hiyo ilikuwa ishara tosha kuwa maisha yao yalikuwa hatarini. "Unakumbuka mwanawe Mzee Kina alivyouawa?" Bi. Katembo alimsaili ingawa hili lilikuwa la balagha.

Ni katika hali hii ya giza gubigubi ndipo walipogundua kuwa wamekanyaga chechele. Baraste hii walioiandama, haikuwa ya kuwafikisha kwao. liliwaelekeza kwa "*Wenyewe*" – Makaburini"!...."Makaburini"? Bw. Katembo aliuliza kwa mshangao. "Naam akili ziliwaduru na **kuwazinga** tena. Kipindi hicho chote wakiwa uchi, vicheko vya watu wasioonekana vilisikika nyuma yao. Ghafla Ng'andu akamparamia na kumdandia Sijali mgongoni. Akapasua unyende ambao nusra uwafufue wafu wenyewe.

Hali hii ya kuatua moyo iliendelea kwa kipindi. Mara vikohozi vya mfululizo kama kwamba watu wenye kifuakikuu, mara kofi za vitanga

vya mikono zilisikika kwa mrindimo wa kupasua masikio ya viduko, mara mbinja na miluzi, mara vilio vya huzuni, majonzi na jitimai. “Uii! Uii! Uii! Ninateketea! Ninachomeka! Ninateseka! Ninaungua! Laiti ningalijua nisingaliiba! Nisingalimsingizia! Nisingalimwonea kijicho! Nisingaliua! Nisingaliwalaghai! Nisingaliiba mtihani! Nisingalijiingiza kwenye fuska za ureda na uroda! Nisingalikuwa fisadi! Nisingaliwaangamiza ndugu na wazazi wangu! Nisingalijihusisha na huo uchawi na usihiri!” Hizi ndizo jumbe za majuto zinazohinikiza ile anga ya maziarani.

Pale chini, Karibu na mti wa mretemu, walijikunyata huku wamefufumaa na kudatama kwa hofu. Roho zao zilisalia mikononi. Laiti ardhi ingepasuka iwameze lakini wapi! Walijizoazoa na kukimbilia kwingineko. Katika hali ya kujiokoa, walijikuta wametumbukia ndani ya shimo kutokana na giza lililoitawala sehemu hiyo. Siku ya nyani kufa miti yote huteleza. Juhudi hizi zikawa sawa na kuruka mkojo na kukanyaga kinyesi! Kwani walijipata kwenye shimo hilo halikuwa shimo la kawaida, bali kaburi lililokuwa limeandaliwa siku iliyotangulia kwa maziko ya kijana mmoja aliyehusika kwenye ajali ya barabara. Ajali iliyotokea kwenye barabara kuu ya Kakuma – Lokichogio karibu na soko la Makuti. Wakiwa wamejibanza na kujificha sehemu moja ya shimo hili, walihisi uwepo wa mtu mle ndani.  Mtu mwenyewe alijinyanyua na kuwakaribia. Alipowafikia, akaanza kuwapapasapapasa na kuwashikashika japo kwa kubahatisha kutokana na hilo giza jingi. Wakajaribu kupiga unyende wakashindwa.

Kwa bahati mbaya au nzuri aliwatambua kwa majina, “Ng’aandu! Ng’aandu! Siijali! Siijali! Siijali! Waa Katembo?” japo alizungumza akidodosadodosa na kusitasita, hao watoto waliitambua sauti hiyo.

Ilikuwa ya mlevi aliyejulikana na kila mkazi kama mraibu na mlokole sugu wa kileo almaarufu ‘*kaada*’ kama kinavyoitwa katika eneo letu" Kabla ya kuendelea na kisa chake, alichachawizwa na Bi Katembo. "Alikuwa akifanya nini mle haswa usiku huo?" "Yaonekana alikuwa humo kwa kipindi kirefu. Huenda ulevi ulimzidi ulampeleka kule. Kwani hata hizo dalili za ulevi na **maruerue** zilikuwa zimemwondoka

Mumo humo ndani, walihadithiana kilichomfikisha kila mmoja pale. Bw. Mtindi kama alivyojulikana, aliwafahamisha kuwa alijikuta humo baada ya kupotea njia kutokana na mazigazi ya ulevi uliomfanya awe chordo. Alikuwa akitoka cheteni kuwanunulia wanawe sare za shule. Sadfa iliyoje?

Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki. Bw. Mtindi aliibukia kuwa wa msaada kwa vijana hawa si tu kwa kuwapa usalama, bali pia kuwasereti uchi na utupu wao. Japo bombo aliyoivaa Sijali ilimpyayapyaya kwa mipyayo nayo ile ya Ng’andu ikambana ajabu, waliona kuwa ni heri madhali, heri shari nusu kuliko shari kamili. Kabla ya kuondoka, mkongwe huyu alidhukuru kuwa alikuwa amejinunulia pia kurunzi.

Inaaminika kuwa roho za mizuka ni adui na hasidi wakubwa wa mwangaza. Mara tu kurunzi ilipowashwa, sauti hizi zilisikika zikienda kwa kasi ya nduma na kutokomea kule kusikojulikana. Hii iliwapa nafasi ya kupumua na kuhisi kuwa kuna uhai tena. Waliongozana unyo kwa unyo na kimya kimya kuelekea nyumbani. Kuntu, ng’ombe akivunjika mguu malishoni hujikokota zizini. Waliwasili kila mmoja kwao dakika chache kufika saa kumi na moja alfajiri wakiwa wamechoka na kunyong’onyea kwa machovu ya mwili na roho.

Yamkini hili likawa funzo chungu kwao baada ya kuwapuuza na kuyapuuza mawaidha ya wazee", Bi Mwaipaja aliwashangaza kwa kisa hicho. Ilimbidi arejee kwake. "Lazima niandamane nawe ili niende nimnasihi mwanambee wangu. Hakuwa mtundu kiasi hicho". Bi Katembo alimjuza.

Walipofika kwa Bi Mwaipaja, Bi Katembo alisimuliwa kisa kicho hicho kutoka mwanzo hadi mwisho na Ng'andu. Aliwaonya kutorudia tena au kuenda kokote pasipo mhuri wa wazaziwo. Kuhusu wenzao walioandamana nao ni kwamba walifika mapema nyumbani. Walipofika, wavyele wao waliwaadhibu na kuwapeleka katika shule ya bweni siku iliyofuata.

Waliendelea kuwanasihi ili wawe kitovu cha maisha mema. Kila siku walipokuwa shuleni hawakuchelea kuhudhuria vipindi vya ushauri nasaha chini ya usimamizi wa Bw. Masumbuko

Jioni ya siku moja ya kabla ya kurejea nyumbani, wanafunzi wote waliitwa kwenye gwaride. Kengele ya dharura ilikirizwa. ‘Si kawaida kuwepo na gwaride hasa wakati huu wa alasiri’ Ng’andu akajisemea huku roho ikimpapa na kumpapatika. Mbiu ya **mgambo** ikilia bila shaka kuna jambo. Mtu hakatai wito, hukataa aitiwalo. Walimu pamoja na wanafunzi wa shule ya St. Stephano walitagusana kwenye gwaride hii kwa hamu ya kutaka kujua kisa na maana.

Naibu wa mwalimu mkuu Bw. Shisundi ndiye aliyetakadamu kwa mazungumzo mafupi, kisha baadaye alimkaribisha mwalimu mkuu Bw. Sitinei – Tambo la mtu. Mwalimu mkuu alikaribishwa kwa shangwe na hoi hoi. Hiyo ilikuwa ishara tosha kuwa alikuwa kipenzi cha wanafunzi wengi. Bw. Sitinei aliitakasa koo na kuwasabahi wanafunzi na walimu.

Mara tu anapohitimisha utweshi, pakatokea kelele, zahama na tandabelua miongoni mwa wasichana waliokuwa karibu na mwalimu wa zamu – Bw. Makini.

Mwanafunzi aliyeanguka chini na kunyooka twa! Si mwingine ila ni Ng'andu. Alizimia na kuzirai. Ghafla povu na fuo linamtoka kinywani, vidole **vikagandamana**, meno yakaumana kama chuma kwenye jiriwa, macho yakabadilikabadilika; mara meupe, mara mekundu: ingawa ule weupe ndio uliotisha na kuatua moyo sana. Jasho likamtiririka ungedhani ni bomba la maji lililopasuka.

Wakati kama huu ndipo kila mbinu na wazo huhitajika ili kuyanusuru maisha hata kama yanaonyesha dalili za kuisha. Bw. Makini pamoja na Bi. Ngereza walimnyanyua Ng'andu kitikiti, chuchulichuchuli na himahima hadi kwenye majilisi ya shule. Licha ya kupewa na kufanyiwa huduma ya kwanza, hali iliendelea kudorora mbayaya na kupindukia. Hapo ndipo nilipogundua kuwa kabla uhai umwondoke kiumbe, roho huwa na vita vikali dhidi ya ulimwengu wa ahera na huu tuliomo.

Ng'andu, mwanaye Bi. Mwaipaja, iliashirishia waziwazi kuwa maisha yake yalikuwa yamening'inia juu ya uzi mwembamba ambao huenda ungekatika wakati wowote. Mara ulimi wake ulijitokeza kinywani ghafla. Hapa palihitajika watu wenye misuli na udole wa kumdhibiti madhali nguvu alizokuwa nazo hazikuwa tofauti na za yule mtu aliyepagawa na aidha pepo mchafu, milihoi au jini.

Tukio, kadhia na kisa mfano huu si cha kupenyea meno. Badala yake, faradhi na sharti yeyote awe na ujasiri, ushakii na ukakamavu ndipo amenyane na kupambana nayo faya kun faya. Walioonekana

kujawa na hawafu nyingi ni wale wanafunzi walianza kulia. Vilio vya kite na vya ndani kwa ndani kwa kutoelewa kuwa hapana siku hata moja kilio kimewahi tumika kama dawa wala suluhu yoyote ya matatizo. Juhudi za mwalimu wa zamu kuwaonya dhidi ya hivyo vilio, ziligonga mwamba kwani wasingeyazuia machozi kudondoka japo kichembachemba na kisirisiri.

Ukweli na uhalisia usiosetirika ni kuwa, Ng'andu aliuthamini na kuuenzi **muamala** na maingiliano mema na kila mmoja pale shuleni. Pengine niseme sintofahamu zinazojitokeza kati yake na wavyele ni zile za maumbile. Maumbile huja eti. Hata hivyo, hakuna mchele ukosao ndume. Ama siseme, hakuna bamvua lisilo na usubi abadan kataan. Ni wakati huu huu ndipo gari la ambulensi linaonekana likiingia kwenye lango la shule kwa mwendo wa spidi ya wastani ingawa taratibu lisije likasababisha matatizo mengine tena. Mlio wa king'ora ndio uliowatahadharisha waja kuondoka mapitoni.

Mjo na mlio wa honi wa ambulensi ulizidisha uchungu, simanzi na jitimai nyoyoni mwa wengi. Hasa wale watoto waliosoma na Ng'andu kwenye darasa moja ndio walioathirika maradufu. Hapa kwetu mlio wa king'ora huashiria mambo mawili ya kutisha. Aidha, kifo au kati ya uhai na kaburi. Wanafunzi wengi walisikika wakilia kwa uchungu na machozi kifua tele "Jamani! Hamadi! Uuii! Uuii! Ng'andu! Ng'andu! Ng'andu! *Please! Please!* Usituache, usiende, Mungu wetu! Mtume simama! Mbona? Mbona? Mbona? *Why? Why? Why take her life*? Harufu ya mauko na huzuni ndizo zilizohinikiza kila mahali. Ghafla, Ng'andu aligeuza kichwa na kuyafumbua macho ambayo sasa ni mekundu kupindukia. Aliwatazama wanafunzi wenzake ingawa kwa huzuni nyingi. Uso wake uliosawijika na kujaa mapakupaku ulitisha sana. Kwa

mujarabu, alipiga chafya kwa sauti ya mfyatuko wa mtutu wa bunduki, “tishyaa!”. kabla ya kuyafumba tena macho, aliunyanyua mkono wa kulia na kuwapungia. Ishara tosha ya ……………… Mwisho kabisa sauti ilisikika ingawa nyonge na dhalili ikiyakariri maneno haya “Ni….lee…tee…ni sii…jaa….li….hu…ko…..ni…e…..nda….ko….

Haya ya Sijali, yalimfikia kila mmoja kwa mduwalizo na kimako kikubwa. “Mbona Sijali? Mbona yeye tu? Kwani pana siri gani kati yake na Sijali?” wengi walisikika wakinong’onezana na kupenyepenye japo mara hii kwa woga na ukunguru wa aina fulani. Yamkini hii ilitokana na huu mjo wa hawa matabibu waliojitoma kwenye ukumbi huu wakiongozwa na mwalimu mkuu Bw. Sitenei. Waliingia wakiwa wamevalia na kujisetiri kwa mavazi aina fulani ya ajabu. Walikuwa wamejifunika kutoka utosini hadi unyayoni. Mavazi yenyewe ni yale ya sandarusi au niseme plastiki. Kwa jumla ni madaktari wanne kila mmoja alibeba vifaa vya kazi; usiende vitani bila silaha!

Mwalimu mkuu aliruhusiwa kusimama hatua kama mbili hivi mbali na mgonjwa kisha tabibu mmoja wao akaanza kumkaguakagua na kumchunguzachunguza kwa kipimajoto. Bila shaka kuthibitisha iwapo maskini Ng’andu yu ngali sayari ya tatu ama amekwisha ng’oa nanga ya safari isiyo na marejeo! Baada ya mazungumzo mafupi na mwalimu, Bw. Sitenei alionekana akitikisa kichwa kwa mshtuko! Huenda ameupokea ujumbe unaohitaji moyo mkuu kuukabali na kustahimili. Habari hii ikasubiriwa na wengi kwa mchanganyiko wa hofu, uchu na **hawaa**. Ndiyo mawazo mchafukoge basi.

Matabibu walimwingiza Ng’andu kwenye ambulensi, dereva akalitia gari mafuta kisha wanaondoka kwa kishindo sawa na jinsi

walivyoingia. Ukweli ni kwamba, wameyaacha nyuma maswali mengi kuliko majibu. “Mbona wakaondoka minghairi ya mwalimu hata mmoja? Mbona wakavalia hivyo?” Haya ndiyo baadhi ya maswali nui yaliyoendelea kuwapiga kumbo na kuwatinga bila huruma wala imani. Wakadurika na kuhasirika pakubwa. Walimu hawakuwa wamemjuza mamaye Ng'andu. Sijali alitimua mbio kupeleka ujumbe huo mzito. Aliwakuta Bi Katembo na Bi. Mwaipaja wakiwa mazungumzoni. Habari hizo zilimshtua sana maana mwanawe alitoka nyumbani akiwa mzima. Baada ya dakika kumi hivi, aliarifiwa kutoelekea shuleni wala hospitalini. Mbona? Ndicho kitendawili.

Tangazo na ilani ya jioni hiyo kutoka kwa mwalimu mkuu ilisheheni **simanzi** na sononeko si kidogo. Ikawafikia wengi kwa mduwalifu, kimako na mtanabahisho wa ibra. Kila nafsi ikawa hoi na taabani kwa kuarifiwa kuwa Ng’andu aligundulika na kupatikana na ukongo hatari wa ‘KORONA’ Hii ikawa wazi kama jua la mchana kwa yeyote aliyetagusana naye kwa njia yoyote ile kuingiwa na tumbo joto. Washukiwa wa kwanza kabisa kusakwa na kutiwa mbaroni ni pamoja na SIJALI ambaye hakujali, wazee wake na wazee wa Ng’andu. Isitoshe, yeyote ambaye angejitokeza kwa madai ya kukaribiana na Ng’andu. Wizara ya afya chini ya ulinzi mkali kutoka serikali kuu, ikatangaza ilani kali ya kumchukulia sheria yeyote ambaye angekaribia shule hii ya St. Stefano. Eneo hili likadhibitiwa kwa siku kumi na nne bila yeyote kutoka wala kuingia.

Bi. Mwaipaja alizidi kuchanganyikiwa zaidi. Hilo tukio lilimfanya Bi Katembo kukawia kuridi kwake . Bi Mwaipaja akiwa amejipweteka kwenye kochi, pale sebuleni baada ya **amali** na hamsini ya kutwa hiyo, Mawazo yalisalia kwa mwanawe wa pekee Ng'andu. Bi Katembo

hakuchelea kumliwaza na kumkomaza. Madakatari walimwarifu kuwa mwanawe alikuwa akiugua uele usiojulikana. Machungu belele yaliyoletwa hasa na ukongo huu hatari na wa kufisha yalimchuna sana Bi Mwaipaja. Alikuwa ametulia na kukimya kwenye kiti kilichoundwa kwa mbao za msonobari; kiti ambacho alirithishwa na baba yake – mzee Ayombera ambaye alisafirishwa ahera juzijuzi mintarafu ya huyu nduli. "Usiwe ni huo ugonjwa wa babako ndio uliomlemea mwanao! Maana naye alikuwa na ishara zizo hizo" Bi Katembo alisononeka kwa kauli hiyo. "Si wewe pekee unavyodhani! Uele huu umenipokonya wazazi wangu wote pamoja na maumbu zangu wanne kwa kipindi kisichozidi miezi miwili", Bi Mwaipaja aliongezea huku machozi yakimtiririka njia mbili mbili.  Rukono inatoka kwenye **kitanga** chake na kudondoka chini bila mwao wake. Hii ilitokana na jinsi **alivyoduriwa** na mawazo mchafukoge.

"Ninapoyatupa macho yangu nje kupitia kwenye dirisha la nyumba, ninayaona kwa huzuni makaburi **tandatu** walimolala jamaa zangu Ninakumbuka wimbo ulioimbwa katika mazishi na maziko ya mama.

*Luwere khulanga mai, Luwere*

*Luwere, Luwere,*

*Luwere Khulanga mai Luwere,*

*Luwere Nyasaye akhulinde………."*

Yaani maana halisi ni kuwa sina wa kuita mama tena! sina wa kuita baba! tena, sina! Sina! Sina! Nitayauguza majeraha na vidonda vya moyo na akili hadi lini" Bi Mwaipaja alizidi kumkumbusha Bi Katembo

namna maisha yalivyomkimbia. "Mungu azilaze roho zao mahali pema **firdausini".** Bi Katembo alimliwaza shogake kwa maneno ya mshamara.

Waliifungulia runinga na kuanza kutazama. Kiwambo cha televisheni kiliwakaribisha kwa picha za vibonzo. Cha kwanza kilijiita UKIMWI, cha pili KORONA na kile cha tatu kikajipagaza DUNIA. Ukimwi na korona walianza kulumbana na kugombana huku wakirushiana cheche za matusi yaliyosheheni dharau, **twezo** na mabezo ya ajabu.

“Wewe umefika hivi juzi ukanipata hapa, ulipewa idhini na nani?” UKIMWI alimkabili KORONA. “kwani wewe ni nani kunidadisidadisi na kunipekuapekua kama polisi?” *Go there*! Kwenda huko! UKIMWI akapokea mzinga wa jawabu. Malumbana na utesi huu unapoendelea, DUNIA anawatazama kwa jicho tu na aidha kwa mshangao bila kusema lolote wala chochote. Yamkini aliufahamu ule ulumbi usemao, “Ukiona neno, usiposema neno hupatikani na neno”

Kumbe mzaha mzaha hutumbua usaha. Kabla ya muda wa kuku kumeza punje kutimilika, pakazuka vita na mapigano makali ya nguo kuchanika kati ya Bw. UKIMWI na Bw. KORONA “Wewe ni sawa na mbwa asiye na meno, kisu butu wewe, unajishasha na **kujishoboa** ilhali ulishindwa kuuangamiza ulimwengu. *You are as useless as a toothless dog*” KORONA akamkejeli, kumdhalilisha, kumthakifisha na kumdunisha Bw. UKIMWI hadharani.

Mie binafsi sidhani iwapo kauli za Bw. KORONA ni za kweli kwani bado Bw. DUNIA anayashuhudia makali na athari za Bw. UKIMWI japo si dhahiri kama hapo awali. Watoto wa Bw. DUNIA wasidanganyike wala kuhadaika. Athari za UKIMWI bado zipo hai na

mzimamzima. Jihadharini msije mkahasirika. Bw. DUNIA anapobainikiwa kuwa Bw. UKIMWI ameinyanyua mikono yake na kupiga magoti kwa ishara ya kusalimu amri, anawakaribia na kuwasihi wasameheane na kuwa radhi kuishi pamoja kwenye makazi haya ya DUNIA! Sijui iwapo hawa wawili walifahamu kuwa sahau ndio dawa ya mja.

Huu ushirikiano uliwapa uhuru na istikilali ya kuwaangamiza waja DUNIANI bila kujali kabila, utaifa, rangi, tabaka; wote maskini na mabwanyenye wakagugunwa na kung'ong'onwa bila kusazwa hata chembe. Hii ndio maana unapoingia DUNIANI, kinachokulaki ni makaburi yaliyojaa roho za waliomezwa na kutafunwa na hawa nduli.

Baada ya kuchoshwa na elimu hiyo ya vibonzo wanapania kuelekea hospitalini alipokuwa Ng'andu baada ya kuamrishwa na madaktari.

Gari la ambulensi liliwasili kwenye lango la hospitali baada ya saa tano. Ng'andu akabebwa moja kwa moja na kupelekwa kwenye mashine ya wagonjwa mahututi. Yalikuwa mashine maalum ya waathiriwa wa KORONA. Kwa zaidi ya siku hamsa wa ishirini, maskini hajaonyesha dalili yoyote ya kupumua japo mwili ungali na chembechembe za joto. Hata wauguzi yamkini wamekwisha enda nguu kuhusu kuishi tena kwa msichana Ng'andu. Lakini Mungu ni nani? Yake ni mengi, ya kuku ni mayai! Ndivyo wasemavyo vijana wa leo. Madaktari hutibu maradhi tu! Hawaponyi. Hutibu magonjwa lakini hawana uwezo wa kutibu kifo. Hii ni dhima ya Mungu mwenye kuumba.

Siku kumi baadaye, manesi walibainikiwa kuwa roho ya Ng'andu imekuwa ikisukuma damu japo kwa mbali sana. Kudura za Mungu pamoja na idili, juhudi na jitihada za wauguzi zikayanusuru maisha ya

msichana huyo. Siha yake ikaendelea kuimarika na kustawi kila kulipokucha na kulipokuchwa. Maulana ana uwezo na udole wa kufufua nyama kitangani.

Walimuuguza hadi akapata afua yake. Siku tatu baadaye aliruhusiwa kwenda nyumbani. Ng'andu alifurahi sana. Moyoni alikuwa na matamanio ya kuwaona tena walimu na wanafunzi wenzake. Bi Katembo alimuomba sahibuye ruhusa ya kurejea kwake ila akamsihi asubiri ili amsaidie kuuguza hali ya mwanawe jambo ambalo alilikubali.

Akiwa amejilaza kwenye godoro alilowekewa kwenye kivuli cha mti huu wa mwembe, mawazo yake yaling'oa habta na kuanza kuyakunjua madhara mengi tu yaliyosababishwa na gonjwa hili la virusi vya Korona. Alijikuta akijisomea orodha ndefu sana kwenye kitabu cha mawazo yake: si wengi kupigwa kalamu, si kudorora kwa uchumi wa nchi, si vifo na mauko ya ghafla, si migogoro ya kifamilia, si utovu na mmomonyoko wa maadili hasa sana miongoni mwa vijana, si ulanguzi na utumizi wa dawa za kulevya, si ndoa za mapema, si mapenzi ya kiholela si uavyaji wa mimba, si kuseleaselea na kudorora kwa viwango vya elimu, si kupanda kwa gharama ya maisha! Mawazo yaya haya yanamfikisha shuleni.

Ni muda wa saa moja hivi, jua limeanza kuirambisha miale yake kwenye janibu za mashariki ili kuibisha siku nyingine. Wanafunzi wanaonekana wakipita kwa marshimarshi ilmuradi wajiepushe na hasira za walimu kwa kufika shuleni wakiwa wamelimatia. Wengi wa hawa wanafunzi ni wa shule ya St. Stephano. Ng'andu akiwa pia miongoni mwao. Sifa za shule hii zilitanda na kutandawaa kotekote kutokana na nidhamu ya hali ya juu. Hii ndiyo sababu iliyochangia pakubwa matokeo

ambayo bila hatihati ni ya kumezewa mate. Shule hiyo ilishikilia utepe na kuibeba beramu ya eneo hili si mara moja si mara mbili. Isitoshe, hii ndiyo shule pekee iliyobobea, **kulula**, kukomaa na kutopea katika nyanja nui zikiwemo: riadha, michezo ya kuigiza, kipute, mashairi, uimbaji wa nyimbo za kitamaduni na usakataji dansi.

Kuntu na yakini, shule hii ilifahamu dafina ya kuyakidhi mahitaji yote ya watoto. Uongozi wa shule hii tajika haukuzingatia tu ujuzi na ufahamu wa vitabu na mitihani bali pia nafasi ya vipaji na talanta za watoto. Ninashuku na kutuhumu kuwa hii ya dansi ndiyo iliyowapa akina Ng'andu na Sijali nafasi na tajriba mahususi ya kunengua, kudengua na kucheza ngoma kwa viuno ungefikiri labda walizaliwa bila mifupa yoyote!

Alijinyanyua polepole baada ya kuhisi haja ndogo. Akaondoka taratibu na kuvivuka vidato vya jengo linalomfikisha kwenye ghorofa ile ya pili ambamo bila shaka ndimo mna vyoo vya kujisaidia. Baada ya kutabawali, alitazama kwenye ukuta na mara jicho lake linakutana ana kwa ana na mchoro wa mwanamume aliyebeba kiserema akienda mwendo wa kasi. Hii ni baadhi ya michoro aliyokutana nayo kwenye vyoo vya sokoni, hospitalini au shuleni. Mimi sijasema makanisani na misikitini! Huu wa leo haudhihiriki bayana **madhali** umechorwa kwa kutumia sijui kama lilikuwa ni kaa la ukuni au chaki au kinyaa!

Anaporejea, anaazimia kupungia unyunyu kwenye sehemu inayoangaliana na angatua ya eropleni. Papa hapa ndipo alipokumbuka tena picha hiyo ya mzee mwenye jembe aliyejitoma shuleni baada ya kukihitimisha kipindi cha kwanza siku hiyo ya Ijumaa, kama kawaida na kaida ya wanafunzi wa St. Stefano, walitulia tuli kaburi kando. Ukimya

na utengemano si tofauti na ule wa ufuoni. Hawa ni baadhi ya wanafunzi nchini ambao kamwe hawakuhitaji jicho la tatu ndipo watekeleze wajibu wao.

Ng'andu alipoanza kuunga siha yake, alimsihi mamake kumpeleka skulini. Upendo wake wa masomo ulimshawishi mamake.

Siku iliyofuata, alipelekwa na mamake, Sijali pamoja na Bi Katembo. "Sijali naomba ujali hali ya mwenzako. Akiomba chochote mwelekeze", Bi Mwaipaja alimwelekeza Sijali. "Sawa mama nitahakikisha amepata maslahi yote muhimu", Sijali alidakia. Baada ya muda wa dakika kama thelathini, unyende na unyange ulisikika kutoka kwenye lango la shule na kuupasua ukimya huu kwa ghafla. Nidhamu, adabu, thafaka na itibari waliofunzwa, inawakumbusha madhara ya kukimbilia kunakotokea hatari. Hivyo, licha ya vurumai na kelele hizi, akina Ng'andu walibaki mumo darasani. Kimya na utuvu vikawa ni kama awali. Shabash! Bila shaka hii ni tabia nyerezi na bulibuli ya kuandama na kuigwa na kila mja.

Ng’andu ambaye kwa kawaida aliketi karibu na dirisha hatua chache kutoka kwenye mlango, alipigwa na butwaa alipoliona jibaba lenye miraba minne likijitoma kwenye lango la shule kwa mwendo wa duma au swara aliyefumwa kwa mshale wa sumu. Mkononi, lilikuwa limebeba jembe lenye mpini. Wakati huu walimu wamejumuika kwenye afisi ya mwalimu mkuu – Bw. Sitenei kwa mkutano wa kila mwisho wa wiki. Ingawa naibu wa mwalimu mkuu – Bw. Shisundi ndiye aliyekuwa hajawasili.

Ajabu, huyu hayawani alikuwa uchi. Alichokivalia pengine ni hiyo ‘suti’ ya Mungu pamoja na tope alilokuwa amejipaka kutoka kwenye

utosi hadi kwenye ukucha wa miguu. Ni jizee lililokula hadi chakula kikamkana kwa jinywa pana. Rangi ya mwili ni hiyo ya weusi uliokoza uliosababisha makaa na mpingo kuulilia ngoa. Upara na kidazi kichwani ni dalili tosha kuwa dau lake karibu kutia nanga ufuoni.

Taraa, lilipofika kwenye eneo la gwaride, lilitazama kulia na kushoto kwa macho ya tahadhari, kisha likatupa jembe hilo pale chini kisha **likauparaga** mlingoti wa bendera ungedhani ni mayonda au ngedere. Mara tu lilipoanza kuimba nyimbo za kitamaduni haswa ziimbwazo kabla ya vita au wakati wa upashaji wa tohara, ndipo walimu waligundua kuwa kuna hatari! Walipomsikiliza kwa makini, waliyasikia maneno yaliyosheheni na kujaa cheche za matusi, **kebehi** na chomba bila tafsida yoyote.

Katika hali hii ndipo walipobainikiwa kuwa alikuwa **chakaramu**. Hayawani huyu anajisahau kuwa yuko juu ya mwongoti. Anaghilibika na kuanza kunengua na kudengua kiuno. Hali ambayo ilimpeperusha kama karatasi na kumbwaga pale ardhini kwa kishindo cha radi. Alichokibusu pale ni lilo hilo jembe. Alikigonga kinywa chake mia fil mia. Meno yote yakatapakaa papo hapo! Huo ulikuwa uchungu wa mwaka! Aliparagaparaga na kubingirikabingirika kwa maumivu na dhiki. Kichaa kilimtoka. Walimu walimsogea ili kumuauni. Kabla ya hatua kumi hivi, walipigwa na **mughma** walipogundua kuwa alikuwa mwenzao; Bw. Masumbuko; mwalimu wa somo la dini na mshauri nasaha. Si tu wanafunzi bali pia walimu wenzake. Mwalimu ambaye hivi majuzi alikuwa amewazika jamaa zake wote kutokana na ajali ya barabarani! Unyende wa masikitiko uliotoka kwa walimu wa kike, ulimzindua na kumbumburusha kutoka pale chini. Alijinyanyua na kulichukua jembe na kuanza kuwaandama kwa hasira ya mkizi. Wote walikimbiza roho zao

na kujisalimishia ofisini. Ukiwauliza walimu wa kike ni vipi walijikuta ndani ya kabati la mwalimu mkuu, watakuambia kuwa hicho ni kitendawili kisichoteguliwa daima dawamu. Walimu wengine wanne wa kiume nao hawakujua jinsi walivyojikuta juu ya dari la ofisi. Naye Bw. Mkuu alijikuta ndani ya tangi akiwa amejivika na kujisetiri kwa gunia la mahindi. Wengine wakajaribu kuuparamia ukuta lakini nguvu zao zikaishia nyangwani.

Wakiwa mle ndani huku roho mikono, Bw. Otoyo anakumbuka kuwa mwalimu Waliaula hayupo! Kumbe walipokuwa wakikimbilia usalama Bw. Waliaula aliusahau mlango na kukimbilia nyuma ya hilo jengo. Bw. Otoyo aliamua kukata pua na kuunga wajihi kwa kutoka nje. Aliyatupa macho yake kwenye uwanja wa shule, alipigwa na mshtuko kwani Bw. Waliaula alikuwa akifuatwa kwa mbio za umeme na mwalimu Masumbuko. Angani ameibeba silaha hiyo hatari tayari kuutoa uhai wa Bw. Waliaula. Bw. Otoyo alimwandama huku akipiga ukemi wa usaidizi uliowavutia walimu wengine pamoja na majirani wa shule.

Mungu wa Bw. Waliaula alijidhihirisha kwani pindi tu nduli huyu alipogundua kuwa amemkaribia kabisa na kulinyanyua tena hilo jembe angani tayari kumpasua kichwa kwa vipande kadhaa akateleza kwenye tope baada ya kuivyoga samadi ya ng’ombe na kudondoka chini kama gunia la viazi. Huku ndiko kuponea tundu ya sindano. Waama, lililoandikwa na Mungu halifutiki! Walimu waliamua kumkamata kikiki kisha wakamfunga ndi na kisha wakampeleka hospitalini. Uchunguzi ulibainisha kuwa mwalimu Masumbuko alikuwa akisumbuliwa na ugonjwa wa mawazo. Bw. Masumbuko alikuwa mkoi wake Bi. Mwaipaja. Walipopata taarifa hizo, walielekea hospitalini. Wakamchukua na kumpa ushauri-nasaha mpaka akapata hisia zake.

Baada ya wiki mbili, Bi. Katembo aliomba kurejea kwake kwani muda wake ulikuwa umetikisa paa.

Alipofika kwake, alimsimulia mumewe yaliyojiri. Taarifa hizo zilimshtua sana Bw Katembo. Walipokuwa kwenye lindi hilo la mawazo, aliipokea simu kutoka kwa makao makuu ya wizara ya kuzuia majanga nchini. Aliarifiwa kuwa alistahili kuelekea Kapweta kuchukua ridhaa ya kiwanja chake kwani serikali iliamua kuitenga sehemu hiyo kwa ajili ya kulijenga bwawa la maji ambayo yangetumiwa kunyunyuzia mashamba. Bw. Katembo na mkewe walilala maskini wakaamka wakwasi. Ama kweli fimbo ya mnyonge mlifi ni Mola.

Ni yakinifu na ikirari isiyosetirika kuwa, kalamu hushinda upanga. Ni kuntu na thibitisho kuwa elimu, ujuzi, hekima nadhari na maarifa ya kuzikabili changamoto za maishani hupatikana kwenye maandishi. Riwaya zina uwezo mkubwa wa kukaripia, kukemea na kugeuza huika, desturi na nyendo potovu na hasi katika jamii bila kuutumia upanga au nguvu.

# MASWALI.

1) Mbona Bw Katembo alifika nyumbani pasipo kumjuza mkewe?
2) Kipi kilichosababisha umaskini katika aila ya Bw Katembo?
3) Toa methali mbili zinazoonyesha mazingira ya kichumba alichoishi Bi Katembo.
4) Toa kisawe cha neno Uhawinde.
5) Mbona mkopo aaliouchukua  haukumsadia Bw Katembo?
6) Kwa nini Serikali ilikataa kuwapa wakazi wa Kapweta vyandarua?
7) Bi Mwaipaja alikuwa na ujumbe upi kwa shogake?
8) Ng'andu na Sijali walikuwa wana wakorofi. Dhibitisha kauli hii.
9) Eleza maana ya akusaidiaye kwenye ndiye rafiki. Rejelea kisa hiki CHOZI LA DAMU.
10) Andika insha ukielezea umuhimu wa elimu

# MANENO MAGENI

- ✓ **Amegona** - kulala usingizi wa pono.
- ✓ **Ajinabi** - mgeni au gharibu.
- ✓ **Kinanahaluli** - aina ya dawa inayomfanya mtu aharishe.
- ✓ **Kadimu** - zamani sana.
- ✓ **Kokoneko** - hofu, hawafu au wasiwasi. Au lia kama afanyavyo kuku.
- ✓ **Kustakiri** - kutulia, kumakinika.
- ✓ **Kusarasara** - kutapakiza kila mahali
- ✓ **Adharusi** - mapigano, vita au kondo
- ✓ **Mauko** - kifo au maafa.
- ✓ **Mafaja-** ua unaozunguka boma
- ✓ **Maghafala-** usahaulifu
- ✓ **Junaa** - aibu, kinamasi, hizaya.
- ✓ **Ukoko hadi ulando-** kutoka mwanzo hadi mwisho
- ✓ **Kifyefye-** mtu aliyekonda. Pia kifefe.
- ✓ **Usuhuba** - urafiki
- ✓ **Mbasi** - mwandani, rafiki au msena.

- ✓ **Wakiovodha** - ogelea juu ya maji.
- ✓ **Zikiwapapa** - Hali ya moyo kwenda kwa kasi.
- ✓ **Ubedui** - ukatili, udhalimu
- ✓ **Kuwazinga** - fanya uasherati
- ✓ Maruerue - hali ya kujihisi dhaifu.
- ✓ **Mgambo** - mkutano wa mambo ya busara.
- ✓ **Viligandamana** - kamatani kikiki
- ✓ **Muamala** - hali ya kuwa na uhusiano mwema.
- ✓ **Hawaa** - kuwa na hanjamu au ashiki ya kufanya kitu.
- ✓ **Simanzi** - kuwa katika hali ya kusononeka.
- ✓ **Amali** - kazi au mazoea.
- ✓ **Kitanga** - tukuu au dugu.
- ✓ **Tandatu**- sita
- ✓ **Firdausini** - peponi panapoaminika kuwa roho za wafu huishi baada ya kufa.
- ✓ **Twezo** - aibu, kuvunjia mtu heshima
- ✓ **Kujishoboa** - kujishaua.
- ✓ **Kulola** - kutazama
- ✓ **Madhali** - maadamu. Kwa kuwa, kwa sababu

- ✓ **Likauparaga** - kupanda mti usio na pandio wala tagaa.
- ✓ **Kebehi** - maneno ya kuudhi.
- ✓ **Mughm** - mshangao.